BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# MUHTASARI WA RIPOTI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia fursa hii adhimu kwa kumshukuru Allah Subuhanahu Wataala, Mwingi wa Rehma na Mwenye Kurehemu, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, kwa kutujaalia afya na uzima na kuweza kutekeleza majukumu yetu ya kila siku kwa hali ya usalama na amani.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti wa Kamati yetu ya Ustawi wa Jamii mbele ya Baraza lako Tukufu. Ripoti ambayo inaonesha shughuli zetu zote ambazo tumezitekeleza katika kipindi kilichopita.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ya Ustawi wa Jamii imeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya 1984 pamoja na Kanuni 107(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020).

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kutumia nafasi hii tena kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii, kwa mashirikiano yao makubwa ambayo yameiwezesha Kamati yetu kufanyakazi kwa ufanisi na uweledi mkubwa. Kwa ruhusa yako sasa naomba niwatambue Waheshimiwa Wajumbe hao pamoja na Makatibu wa Kamati kama ifuatavyo:-

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| 8. | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| 9. | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utaratibu uliowekwa katika kazi za Kamati kwa muda wote uliopita, Kamati yetu ilipanga kufuatilia utekelezaji wa malengo na majukumu ya Wizara zifuatazo:-

1. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
2. Wizara ya Afya.
3. Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.
4. Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa mwaka huu wa fedha 2022/2023, Kamati ya Ustawi wa Jamii ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki sita (6) baina ya Unguja, Pemba na Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo, sasa naomba nianze kuwasilisha Muhtasari wa Ripoti ya Kamati hii ya Ustawi wa Jamii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kama

inavyoelekezwa na Kanuni 109(15) ya Kanuni za Kudumu za Baraza (Toleo la 2020).

## WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina Programu Kuu Sita (6) ambazo zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa ya utatu, yaani baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje. Programu hizo ni:-

(i) Programu Kuu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
(ii) Programu Kuu ya Elimu ya Sekondari;
(iii) Programu Kuu ya Elimu ya Juu;
(iv) Programu Kuu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;
(v) Programu Kuu ya Ubora wa Elimu; na
(vi) Programu Kuu ya Utawala na Uongozi.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA JUU

## CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

**Mheshimiwa Spika,**

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chuo hiki kilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 sambamba na marekebisho ya Sheria ya Chuo, Nam. 11 ya mwaka 2009. Sasa Chuo hiki kinakabiliwa na changamoto nyingi za uendeshaji katika Skuli zote inazozisimamia ikiwemo Skuli ya Sayansi na Tiba ya Afya, Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Mafunzo ya Habari, Skuli ya Biashara, Skuli ya Kilimo na Skuli ya Utalii.

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa changamoto hizo ni uwepo wa mishahara midogo ndani ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kulinganisha na Vyuo au Taasisi nyengine,

suala hii linapelekea wanataaluma wengi kuchukua likizo bila ya malipo kwa ajili ya kutafuta maslahi yaliyobora nje ya Chuo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na changamoto hiyo, Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaongezea bajeti ya mishahara Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ili wafanyakazi waweze kufanya kazi kwa ufanisi na kuondokana na dhana ya kutafuta maslahi bora katika vyuo vya nje.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, changamoto nyengine inayowakabili Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) ni uwepo wa madeni makubwa yanayotokana na walimu wa muda (part timers) wanaosomesha katika Skuli mbali mbali zilizopo chini ya Chuo Kikuu hicho.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa kipindi cha robo ya pili (Oktoba - Disemba) kwa Skuli ya Sayansi na Tiba za Afya (Mbweni) imetumia jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja Hamsini na Nane, Laki Moja na Sitini na Nne, Mia Tatu na Thelathini na Nane (158,164,338,000/=) kwa kuwalipa walimu wa muda mfupi, hali inayopelekea fedha nyingi inayotengwa kwa ajili ya matumizi ya shughuli za uendeshaji wa Skuli zinatumika kwa kuwalipa walimu hao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Skuli ya Biashara (Chwaka) Kamati inaendelea kuishauri tena Serikali kama ilivyoshauri katika Ripoti iliyopita ya mwaka 2021/2022 kuiomba Wizara ya Fedha kukaa pamoja na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitafutia ufumbuzi suala la deni linalotokana na Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia ya Wanafunzi katika Kampasi ya Chwaka lililojengwa na ZSSF. Jengo hilo hivi sasa hali ya hairidhishi na deni bado halijamalizika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, katika utekelezaji wa majukumu yake imebaini uwepo wa changamoto kubwa katika suala zima la utumiaji wa Mfumo Mpya wa Manunuzi ulioanzishwa chini ya Mamlaka ya Manunuzi na kupelekea miradi mingi iliyotengewa fedha za Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) kuchelewa kuanza kutokana na upya na ugumu wa kuingia kwenye mfumo huo. Hivyo, kupelekea Zabuni kuchelewa kutangazwa na baadae kupata Mzabuni kwa haraka na kupelekea kuongozeka kwa gharama za matumizi.

## PROGRAMU KUU YA ELIMU YA SEKONDARI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati ilipata nafasi ya kufanya ziara Skuli Ufundi Mikunguni. Miongoni mwa tuliyaona ni uhaba wa watendaji wenye ujuzi na taaluma juu ya fani za Ufundi Seremala, Sehemu ya Ufundi wa Kuchomea Vyuma (Welding). Hii imetokana na walimu wengi kufikia muda wa kustaafu na hakuna walimu wapya waliojaza nafasi. Hali hii imepelekea wanafunzi kukosa utaalamu wa kutosha.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora wanapotangaza nafasi za ajira ni vyema kuzingatia nafasi zilizowazi za uajiri wa wataalamu wenye fani na taaluma zinazohitajika katika Skuli ya Sekondari ya Ufundi Mikunguni ili kuondoa kadhia ya ukosefu wa wataalam wa masomo katika Skuli hiyo.

## PROGRAMU KUU YA UBORA WA ELIMU

**Mheshimiwa Spika,**

Katika programu hii, Kamati imebaini kuwepo kwa uhaba wa madarasa ya kufundishia na kujifunzia wanafunzi katika Skuli ya Msingi Michakaini Pemba, hali inayowasababishia wanafunzi hao kuingia mikondo miwili na wengine kusoma chini ya miti na ndani ya Msikiti. Vile vile, Kamati imebaini uhaba wa walimu na vitendeakazi katika ufundishaji wa Elimu Mjumuisho.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kwa mwaka wa fedha unaokuja 2023/2024 kutenga fedha maalum za ujenzi wa Skuli ya Msingi mpya ya Michakaini Pemba kwani kwa sasa Skuli hiyo imechakaa sana na haikidhi mahitaji yaliopo kwa kuwepo idadi kubwa ya wanafunzi wapatao 4200 ikijumuisha na elimu mjumuisho.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, Kamati inaishauri tena Serikali kuendelea kutoa mafunzo na motisha kwa walimu wa Elimu Mjumuisho kwani wanafanyakazi kazi katika mazingira magumu.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Wizara, Kamati inachukua fursa hii kuipongeza Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa juhudi kubwa wanazoendelea kuzichukua katika kufanya ukarabati wa Madarasa na Majengo ya Skuli mbali kwa Unguja na Pemba katika kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira rafiki na salama. Kamati, inaipongeza tena Wizara kwa kuweza kujenga Majengo mapya ya ghorofa 11 na ujenzi wa madarasa 2100 katika kila Mikoa yote ya Unguja na Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Licha ya juhudu kubwa za Serikali wanazoendelea kuzichukua katika kuhakikisha Sekta ya Elimu inaimarika, Kamati katika ziara zake za ufuatiliaji imebaini changamoto kadhaa katika ujenzi wa Miradi ya Skuli hizo ikiwemo kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha katika miradi yote inayoendelea kutekelezwa kupitia fedha za UVIKO – 19, hali iliyopelekea Wizara kuwa na ongezeko la fedha la jumla ya Tanzania shilingi Bilioni Kumi na Tano (15,000,000,000/=) zinazotokana na kazi za ziada (Variations) mbali na fedha za awali walizopatiwa jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Sitini na Nane (68,000,000,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kuunda Kamati Maalum ya Ufuatiliaji wa Utekelezaji wa Mikataba inayoingiwa baina ya Serikali yetu na Wakandarasi mbali mbali kwa lengo la kujenga usimamizi imara na madhubuti kwa wataalamu wetu wa ndani kwani Kamati imebaini ongezeko hili la ziada linatokana na uelewa mdogo wa wasimamizi wetu wa ndani wa miradi katika shughuli za ujenzi na tathmini ya Miradi mikubwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kukiimarisha Kitengo cha wahandisi wa ndani wa Wizara pamoja na Watu wa Manunuzi kwani Kamati imegundua kuwa ongezeko lote lililojitokeza katika miradi hii ya ujenzi wa madarasa na skuli umechangiwa kwa kiasi kikubwa na uhaba wa wasimamizi na kutokuwa na utaalamu wa kutosha katika masuala ya usimamizi wa ujenzi wa miradi mikubwa na mingi kwa wakati mmoja.

## WIZARA YA AFYA

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Afya ni moja kati ya Wizara muhimu katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ambapo Wizara hii inagusa moja kwa moja afya za wananchi wa Zanzibar. Sambamba na hilo, Wizara hii ina dhamana kubwa ya kuhakikisha kwamba wananchi wote wanafaidika na huduma bora za afya zinazotolewa katika Vituo vya Afya pamoja na Hospitali zetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika kipindi chote cha kazi zake imesimamia utekelezaji wa bajeti inayotumia muundo wa programu katika utekelezaji wake, ambapo kwa Wizara ya Afya kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara hii ilitekeleza na programu zifuatazo:-

(i) Programu Kuu ya Kinga na Elimu ya Afya;
(ii) Programu Kuu ya Huduma za Tiba;
(iii) Programu Kuu ya Uratibu na Uendeshaji wa Wizara ya Afya; na
(iv) Programu Kuu ya Hospitali ya Mnazi Mmoja.

Programu hizo zinatekelezwa kupitia Wizara ya Afya ambapo jumla ya Idara Tano (5), Taasisi Tano (5) na Mabaraza saba (7) ya Taaluma mbali mbali za Kiafya.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Programu zilizopangwa pamoja na kubaini changamoto mbali mbali zinazokwamisha utekelezaji wa shughuli katika sehemu hizo na kuziwasilisha Serikalini kwa kuishauri Serikali namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu changamoto hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kuwepo kwa asilimia kubwa ya watendaji wa mkataba katika Divisheni ya Huduma za Afya ya Akili Hospitali ya Kidongochekundu wanaolipwa na wafadhili ambao itakapomaliza programu hiyo divisheni hii itakuwa haina mfanyakazi wa kudumu hata mmoja. Aidha, Kamati imebaini uhaba wa wataalamu kwenye Sekta hii ya Afya ya Akili

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na Ukosefu huo, Kamati inaishauri Serikali kukaa na Wizara ya Afya kuliangalia kwa kina suala la ukosefu wa watendaji wa kudumu wa Serikali katika Divisheni ya Afya ya Akili Hospitali ya Kidongo Chekundu ambao wanatoa huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofika hapo, kwani Kamati imebaini kuwa watendaji waliopo asilimia kubwa wameajiriwa kwa mkataba na kulipwa na Mfadhili.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, tunaishauri Serikali kuajiri wataalamu bingwa kwenye sekta hii kwani hivi sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la wagonjwa wa afya ya akili.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, kwa upande wa Kitengo cha Afya Kazini Kamati imesikitishwa kwa wafanyakazi wa Kitengo hicho kutokuwa na vitambulisho hali inayowapelekea kufanya kazi katika mazingira magumu haswa pale wakati wanapokwenda kufanya ukaguzi katika maeneo ya Mahoteli, Makampuni na Taasisi Binafsi kuzuiliwa kuingia au kufukuzwa kabisa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Afya kwa kushirikiana Kitengo cha Afya Kazini kuharakisha upatikanaji wa vitambulisho vya kazi kwa wafanyakazi wao ili kuwasaidia kutambulika wanapokagua au kutembelea maeneo yoyote ya kazi kwa ajili ya kufanya kazi zao bila ya vizuizi na kwa ufanisi ikiwa Serikalini au Sekta Binafsi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika kufuatilia utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba, 2022 imegundua kuwepo kwa changamoto ya uletwaji wa dawa za misaada katika Bohari Kuu ya Dawa usiofuata uratibu wa Sheria zilizopo ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Afya kwamba misaada yote inayoletwa kutoka kwa Wahisani mbali mbali kwenda Bohari Kuu ya Dawa ifuate utaratibu uliopo chini ya Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali ili kuepusha uingizwaji wa dawa zilizomaliza muda wa matumizi kwa binaadamu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Taasisi ya Utafiti wa Afya (Binguni), Kamati imesikitishwa na ucheleweshaji wa malipo ya ununuzi wa samani za ofisi (furnitures), ambapo jumla ya Tanzania shilingi Milioni Mia Mbili na Hamsini na Tisa, Laki Sita na Themanini Elfu (259,680,000/=) wanadaiwa na "Darworth Manufactures" ambao ndio wasambazaji. Samani hizo zilipokelewa tangu mwezi wa Disemba, 2021 na barua ya kuomba kufanyika kwa malipo ilitoka kwa Katibu Mkuu Wizara ya Afya kwenda kwa Katibu Mkuu Tume ya Mipango tangu tarehe 08/02/2022, lakini mpaka tunapokea taarifa hiyo malipo hayo bado hayajafanyika. Aidha, Taasisi imepokea barua kutoka kwa wasambazaji kukumbushia deni lao hilo na kutoa taarifa kuwa watachukua samani zao hizo ikiwa hawatalipwa haki yao.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na hali hiyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwapatia fedha Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa ajili ya kufanya malipo ya samani ambazo wamezikopa kwa wasambazaji kwa muda mrefu kwa lengo la kuboresha mazingira ya utendaji kazi wa ofisi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini kuwepo kwa ongezeko kubwa la fedha katika miradi yote inayotekelezwa na Wizara ya Afya kupitia fedha za UVIKO - 19 hali iliyopelekea Wizara kuwa na ongezeko la fedha la Bilioni Ishirini na Moja (21,000,000,000/=) zinazotokana na (Variations) mbali ambapo fedha za awali waliopatiwa ni Bilioni Themanini (80,000,000,000/=) kwa ajili ya Ujenzi wa Hopitali Kumi (10) za Wilaya kwa Unguja na Pemba na Moja (1) ya Mkoa.

**Mheshimiwa Spika,**

Hivyo, Kamati inaishauri Serikali inapotekeleza Miradi mikubwa ya Maendeleo kuwashirikisha kikamilifu wataalamu wa Wizara husika hasa kwenye michoro ili kuepusha changamoto ya matumizi yasiyopangwa ya fedha za Serikali kwa kuwepo ongezeko la kazi za ziada nje ya mkataba waliokubaliana awali.

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ni miongoni mwa Wizara 18 za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Awamu hii ya Nane. Wizara hii inatekeleza shughuli zake kwa kuzingatia mpangilio wa Programu Kuu Tatu na Programu Ndogo Tano katika Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Programu zenyewe ni hizi zifuatazo:-

1. Programu Kuu ya Hifadhi ya Jamii.
2. Programu Kuu ya Utawala na Uendeshaji.
3. Programu Kuu ya Maendeleo ya Jamii na Jinsia.

## PROGRAMU KUU YA HIFADHI YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa utoaji wa Pencheni Jamii kwa Wazee, Kamati imebaini kuwa Wazee wengi wanaopokea Pencheni hiyo kutokuwa na vitambulisho na hata kwa waliokuwa navyo hivyo vitambulisho vimekuwa vikionesha umri mdogo tofauti na umri halisi wa mnufaika au mlengwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na Kadhia hii, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la upatikanaji wa vitambulisho vya Wazee waliofikia umri wa kupokea Pencheni hiyo kwa lengo la kusaidia fedha za Serikali zitumike kwa uadilifu kwa walengwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Pamoja na hayo, suala jengine ni kutumika vibaya Vibali vya Ruhusa (Power of Attorney) kwa watu wanaowawakilisha wazee wao wasiojiweza na wenye mazingira magumu. Kwani baadhi ya wakati wanufaika huwa hawapati stahiki zao na wengine wameshafariki.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika suala hili, Kamati inapendekeza kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kufuatilia pamoja na kuhakiki Vibali vya Ruhusa (Power of Attorney) vyote kwa watu ambao wanaopokea Pencheni Jamii kwa niaba ya wazee wao ili kuokoa fedha za Serikali inayopotea mikononi mwa watu wasiostahiki na kuepusha udanganyifu wa matumizi ya vibali hivyo kinyume na utaratibu wa Sheria.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA

**Mheshimiwa Spika,**

Sambamba na hilo, Kamati imebaini kutokuwepo kwa mashirikiano baina ya Waratibu wa Shehia na jamii haswa katika kushughulikia kesi zinazohusiana na

masuala ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto hali inayopelekea waratibu hao kukosa morali wa kuendelea na kesi hizo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kwa Taasisi za Serikali na Binafsi pamoja na jamii kwa jumla kuongeza mashirikiano katika kupiga vita vitendo vya ukatili na udhalilishaji wanawake na watoto vilivyoshamiri katika jamii kwani mashirikiano ya pamoja ndio yatakayoondoa kabisa vitendo hivyo katika jamii zetu, Wahenga wamesema *"Umoja ni Nguvu na Utengano ni Udhaifu"*.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA UENDESHAJI WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imesikitishwa na gharama kubwa ya ulipaji wa kodi ya jengo la ZSTC (Kinazini) ambalo linatumika kwa matumizi ya Ofisi kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ambapo kwa mwaka wanalipa jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Sitini (60,000,000/=) kwa vyumba vichache visivyotosheleza mahitaji ya Wizara. Hivyo, kupelekea baadhi ya watendaji kuwa na ofisi sehemu tofauti ambapo kwa sasa Mhasibu Mkuu wa Wizara yupo Sebleni, Naibu Waziri yupo Mwanakwerekwe na baadhi ya watendaji kuwepo Welezo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati katika hili, inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia eneo la ujenzi wa jengo la Wizara ili kuondokana na changamoto ya kukodi majengo kwa gharama kubwa pamoja na kusaidia watendaji kufanya kazi katika mazingira rafiki, tulivu na salama kwao.

**Mheshimiwa Spika,**

Ukosefu wa usafiri kwa Wakurugenzi wa ndani ni changamoto nyengine inayoikabili Wizara hii, hali inayopelekea gari iliopo ya Katibu ambayo ni chakavu kutumika kwa ajili ya ufuatiliaji wa masuala ya Wizara nzima.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuwaingizia fedha Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya ununuzi wa magari pamoja na vifaa vya ofisi ili kuwapunguzia usumbufu viongozi wetu pamoja na watendaji wa Wizara hii.

## WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inatekeleza majukumu yake kupitia Programu Kuu Nne (4) ambazo ni:

(i) Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapishaji;

(ii) Programu ya Maendeleo ya Vijana;

(iii) Programu ya Maendeleo ya Utamaduni, Sanaa na Michezo; na

(iv) Programu ya Uendeshaji na Mipango katika Sekta ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPISHAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imebaini uwepo wa mapungufu kwenye Muundo wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ambao hadi sasa hautambui uwepo wa nafasi ya Mkurugenzi wa Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam hali inayopelekea kukosa haki zake za msingi pamoja na stahiki zake nyengine zilizopo kwa mujibu wa Sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, changamoto ya ikama kwa wafanyakazi nje ya Zanzibar wa Dar-es-Salaam na Dodoma hasa kuhusu wenza wao na makaazi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi Serikali kulikamilisha kwa hatua zilizobakia suala la marekebisho ya mapendekezo ya Muundo mpya wa Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC) ili kuweza kutambua baadhi ya nafasi ambazo katika Sheria ya mwanzo hazikuwepo. Mfano halisi, nafasi ya Mkurugenzi Kituo cha ZBC Dar-es-Salaam ambapo nafasi hii inatumikiwa kinyume na matakwa ya Sheria iliyoanzisha Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Pia, kutokuwepo kwa Kanuni ya Utumishi wa Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) Nam. 4 ya mwaka 2013, hali inayosababisha utekelezaji mgumu wa baadhi ya majukumu yao ya kila siku ya Shirika hilo.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na mapungufu hayo, Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuharakisha utungaji wa Kanuni ya Sheria ya Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC) Nam. 4 ya mwaka 2013 kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Shirika hilo ambapo kwa sasa mambo mengi yanakwama na kushindwa kutekelezeka kwa sababu ya kukosekana kwa kanuni hizo. Aidha, Kamati inaishauri Wizara kupitia upya Sheria hiyo ya ZBC ili kuondoa migongano ya kimajukumu baina ya Wizara, Bodi na Shirika.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, imebaini vile vile kuwepo kwa madeni makubwa na ya muda mrefu katika Shirika la Magazeti, hali inayowasababishia kushindwa kufikia malengo waliojipangia ya makusanyo makubwa ya Serikali. Kuna baadhi ya madeni yameshakuwa ni ya muda mrefu tokea mwaka 2016 na hadi sasa taasisi hizo

baadhi yao kushindwa kufanya marejesho yoyote ya malipo hayo. Hadi kufikia Disemba, 2022 Shirika linadai jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja na Sabini na Tatu, Laki Tano na Sabini na Sita, Mia Mbili na Hamsini (173,576,250/=) kati ya fedha hizo jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Moja Ishirini na Tano, Laki Saba na Arubaini na Sita, Mia Mbili na Hamsini (125,746,250/=) zinadaiwa taasisi za Serikali na Binafsi zilizopo Zanzibar. Aidha, jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Arubaini na Saba, Laki Nane na Thelathini (47,830,000/=) zinadaiwa kwa Taasisi za Serikali na Binafsi ziliopo Tanzania Bara. Aidha, jumla ya deni inalodai Shirika hadi kufikia kipindi hiki ni Tanzania Shilingi Bilioni Mbili, Milioni Nane na Sitini na Tano, Laki Moja na Tisini na Sita Elfu (2,865,196,000/=).

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Shirika la Magazeti Zanzibar kusimamia maamuzi yaliotolewa na Serikali juu ya suala zima la ulipwaji wa deni hilo kubwa la usambazwaji wa magazeti kwa Taasisi zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Taasisi na Kampuni Binafsi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Kamati inasikitishwa na suala la kutopatikana kwa fedha za Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Uchapaji zilizoidhinishwa katika makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilipohoji imeelezwa kuwa jitihada zinatumika ila changamoto kubwa ni upatikanaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha. Hivyo, Kamati imeshindwa kufahamu kwani fedha hazijapatikana hadi sasa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kutokana na ucheleweshaji huo, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Afisi ya Rais, Fedha na Mipango kulipa kipaumbele suala la ununuzi wa

mitambo mipya na ya kisasa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji kwani fedha hizo zimeidhinishwa na Baraza la Wawakilishi katika bajeti ya mwaka 2021/2022 – 2022/2023 hadi sasa fedha hizo upatikanaji wake umekuwa wakusuasua na kuwepo kwa majibu yasio na uhakika juu ya upatikanaji wa fedha hizo. Hivyo, kuwafanya Wakala kutumia mitambo kwa muda mrefu bila ya kupumzishwa au kufanyiwa “service” na hatimae baadhi ya mitambo hiyo kuharibika na kupelekea kuikosesha mapato Serikali yatokanayo na huduma za uchapaji.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati, imeendelea kusimitishwa kwa Tume ya Utangazaji kutokuwa na jengo lake na badala yake fedha nyingi za Serikali zinatumika kwa ajili ya kukodi jengo la binafsi kwa matumizi ya Ofisi hiyo ambapo takribani jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Thelathini na Tatu na Laki Moja na Ishirini Elfu (33,120,000/=) hutumika kwa mwaka kukodi jengo la mtu binafsi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia eneo la kujenga ofisi ya kudumu Tume ya Utangazaji Zanzibar ili kuondokana na malipo makubwa ya kodi ya majengo ya watu binafsi.

## PROGRAMU KUU YA UTAWALA NA UENDESHAJI WA WIZARA

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upande wa Wizara, matumizi ya fedha za Ujenzi wa Ukarabati na Uboreshaji wa Kiwanja cha Gombani kuongezeka maradufu tofauti na bei iliyokubalika awali (variations) ni changamoto kubwa hali inayopelekea hadi sasa uwanja huo kusuasua kwenye ujenzi wake.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuliangalia kwa kina suala la ongezeko la matumizi ya ziada katika Mradi wa Ukarabati wa Uwanja wa Gombani (variations) ambapo ongezeko hilo Kamati imegundua limetokana na kutokuwepo kwa michoro ya awali ya uwanja huo na wakandarasi kuomba kwa malipo ya viwango (BOQ) ambayo yalikuwa hayajakamilika yaliyotolewa na Wizara wakati wa kutangaza Zabuni.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati pia inasikitishwa kutokamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya vitano (5) ambavyo ni Kishindeni, Kangani, Mkokotoni, Kitogani na Kama, ambapo Mradi huo umechukuwa muda mrefu tokea 2019/2020 hadi bajeti hii. Pia Kamati inasikitishwa na kutokuwepo kwa majibu ya mazuri ya uendelezaji wa Mradi huo kutoka Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaishauri Serikali kuipatia fedha za Miradi ya Maendeleo Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo ili iweze kutekeleza na kukamilisha miradi hiyo kwa wakati. Katika kipindi hiki cha Oktoba hadi Disemba fedha zilivyoidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka 2022/2023 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ilikuwa ni jumla ya Tanzania Shilingi Bilioni Ishirini na Tatu, Laki Nane na Ishirini na Tisa (23,829,000,000/=) hadi kufikia Disemba, 2022 fedha zilizopatikana ni jumla ya Tanzania Shilingi Milioni Mia Tano na Sitini (560,000,000/=) sawa asilimia 2.4.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa ujumla, Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar imefanikisha majukumu yake ya kufuatilia utekelezaji wa kazi zake katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara hizo ambazo zimeainishwa katika ripoti hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Aidha, Kamati kwa dhati kabisa inachukua nafasi hii adhimu kuzipongeza Wizara na taasisi hizo, kwa juhudi wanazozichukuwa katika utekelezaji wa majukumu ya kazi zao za kila siku. Sambamba na hilo, Kamati inaipongeza Wizara hii kwa kutupa mashirikiano yakutosha kwenye ufuatiliaji wa majukumu yetu ya kazi, Hivyo, inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe zaidi katika kipindi kinachoendelea.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho kabisa, Kamati inatoa shukurani maalum kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi, Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, Katibu wa Baraza la Wawakilishi pamoja na watendaji wote wa Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi mzuri. Mola tunamuomba azidi kutupa mashirikiano zaidi na upendo baina yetu ili kumsaidia Mhe. Rais kwenye kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2025 na Dira ya Maendeleo 2050.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya maelezo hayo ya Muhtasari wa Ripoti, naomba kutoa hoja.

Ahsante,

…………………………..,

Mhe. Mohamed Ahmada Salum,

Mwenyekiti,

Kamati ya Ustawi wa Jamii,

Baraza la Wawakilishi,

**Zanzibar.**